(Ni asubuhi katika mji wa Masisi, Hospitalini Daktari anazunguka zunguka ofisini mwake huku akijizungumzia. Anagutushwa na mwito wa Muuguzi, ambaye anamwita huku akiingia ndani ya ofisi)

Muuguzi : Daktari! Daktari-i-i!

Daktari : (anagutushwa) kuna nini tena?

Muuguzi : Daktari, nimeshindwa la kufanya, yaani ninasikitiko kubwa sana moyoni mwangu...

Daktari : (kwa ukali) eeh! mbona kunishitua bure kama hauna hata la kusema... sinimesha wahi kukukataza tabia kama hizo.

Muuguzi : samahani kukushitua, lakini mimi nimeshindw tufanyeje? Hospitalini mwetu mimejaa wagonjwa, leo asubuhi kumefika hamsini, wengi ambao kama kawaida ni wamama ambao wamebakwa pamoja na watoto ambao ni wagonjwa tokana njaa...

Daktari : oh! ni hatari, nimeshindwa pia. Hapa ulipoingia nilikua nafikiri kuhusu hali ilivyo nchini mwetu. Mbona tunateseka hivi. ubakaji, ufisadi, magonjwa na mabaya yamezidi haswa hapa Mjini Masisi. Sijui tutafanya nini.

Muuguzi : Mimi sasa umefika wakati wa kuinua mikono; hakuna tunachokifanya hapa hospitalini

kama kila siku hivi karibuni watu kumi wanapoteza maisha yao tokana na haya matatizo tuliyo nayo. Hakika naumizwa sana kuona wezetu wakifa na kutendewa kama wanyama. Hebu, fikiria vile hua unahisi pindi unapomona hata mtoto mdogo aliyeharibishwa kupitia ubakaji. Nina uchungu mwingi sababu hakuna linalofanyika kubadili hali bali hali inaendelea kuharibika.

Daktiri : Nakupata mwenzetu, nakuelewa na kuchangia huo uchungu. Mwenyewe vilevile nahuzunika lakini huzuni yangu kuu ni kwamba watu wanafia mikononi mwetu hapa hospitalini; si hata katika mikono ya wahuni ambao hueneza ubakaji na ukora. Endapo tunajitolea kusaidia na kufanya yote tuwezao, Hospitali yetu haina dawa na vifaa vya rahisicha matibabu. Sio muda mwingi uliopita niliandikia Baraza la Mji kuhusu hali hii bali mwenyewe sunajua viongozi wetu vile ni wagumu kutusikiza.

Muuguzi: Shida kabisa, siungewaambia kwamba Hospitali sasa ina wiki mbili bila dawa na kwamba watu wameisha.

Daktari : Nilieleza na kubainisha yote wana Masisi tunapitia kwa undani kabisa, kwanza

waahidi watatoa pesa za kununua dawa wiki iliyopita lakini hawa kutoa chochote Nilipowapigia simu wakaniambia bado pesa ziko katika hatua za kutolewa ambazo sijui inachukua muda gani.

Muuguzi: Asante Mungu! walikubali? Hapo sasa ninatumaini! Mwenye matumaini hafi sababu hata kama ubakaji unazidi tutapiganisha na kuokoa waadhirikaji sababu tutakua na vifaa na dawa za kusaidia kutokana na hizo pesa pindi watakapozitoa.

Daktari: (anashangazwa na maneno ya Muuguzi) Kwani wewe ni mgeni wa Masisi, haujui vile ni wa fisadi na waongo.

Muuguzi: Lakini mbona wameahidi, kwa hiyo wacha tushikiliye hiyo ahadi. Zaidi ya hayo kwani hao viongozi wao sio wanadamu, siwatusikiliy huruma. Licha ya hayo wao ndio viongozi wa jamii sisi ni watu wao.

Daktari: Hatupaswi kuwa kama wajinga. Usiamini kila sauti, haswa ya viongozi wa Masisi. Kwani tumeshuhudia ahadi zao za uongo mara ngapi. Shule ngapi hapa zimefungwa sababu wazazi wameshindwa kulipa karo, huku hao viongozi wakiahidi kulipia watoto wa shule za msingi.

(akiashiria kwa vidole) miaka mitatu sasa tangu waahidi. Uongo mtu! Siwaamini hao hata kidogo!
(Mlango unapigwa kwa nguvu kana kwamba kuna mwenye anataka kujiingisha kwenye nguvu. Nje kuna sikika mtu anayelia)

Muuguzi : Ingia mara moja!

Baba Amina (akihema) Ndugu zangu tafadhali nisaidi.e.ni....

Muuguzi : Tukusaidie nini? Kunanini?

Baba Amani: Mwanan-gu-u...

Daktari : Nini na mwanako bwana we?

Baba Amani: anakaribia kufa, hata hapumui vizuri!

Daktari Nini haswa kilifanyika?

Baba Amina Tafadhali Daktari, mtoto atafariki, njoo uone alafu umsaidie, nakuomba.

Daktari Nakuelewa, lakini lazima tujue kilichofanyika ndio tujue namna gani ya kuliendea. Hebu, Muuguzi wasaidie walete huyo mtoto ndani tumtazame.

Muuguzi Sawa Daktari. (Wanaleta mtoto ndani pamoja na mamaye ambaye analia)

Daktari : (akina na kalamu na daftari mezani mwake) Nahitaji mniambie jina na umri wa mtoto.

Baba Amina Anaitwa Amina, alizwali miaka minne iliyopita.

Daktari Haya, anashida gani mwanako?

Mama Amina: Anashida kubwa sana, Amina leo alitoka nyumbani kucheza na wenzake, huko wahutu wakamkimbiza na kumshika. wanaume tano

ndio naliombaka. Nijambo la kuogofya sana.

Daktari: Nini? ooh! pole sana. Hao watu hao mbona kutuonea hivi? Msinue na wasi nasi tutafanya lolote tuwezalo kumsaidia, huenda akaishi. Hebu mpeleke mke wako nje na mtuache tumfanyiye mtoto uchunguzi ndio tujue namna nzuri ya kumshughulikia (mlango unafungwa, Daktari anachukua pima joto na wanaanza kumpima Amina)

Muuguzi: Daktari vipi, bado anapumua?

Daktari: Anapumua lakini wajua mtoto kama huyu kwa wanaume tano si'o jambo la mchezo. Anabahati sababu hakufariki pindi alipotendewa hivyo. Nashindwa tumsaidie je. Hatuna dawa Zahanatini endapo tutamlaza. (anafikiria..)

Muuguzi: Wajua shida siku hizi ni kwamba hata uchumi wa nchi nao umezorota, watu hawana pesa. Tutalazaje mtu huku tukijua hawana pesa ya kulipia gharama ya matibabu?

Daktari: Kwa hali kama hii, kufikiria juu ya pesa sio muhimu, ni kuokoa maisha kwanza hayo mengine baadaye. Wema hauozi unavyomwona mtoto huyu sasa haujui siku zijazo atakuwa nani na atasaidia jamii vipi. Hata

hivyo hatuna dawa za kulipia. Hebu nenda ukamchamshie maji, halafu ulete vifaa tumwoshe. (anafikiria) hebu weka vijiko mbili vya chumvi ndani ya hayo maji moto ya kumwosha. Nafikiri chumvi utasaidia vidonda hivyo kupata nafuu. (Muuguzi anaondoka kutekeleza kama alivyoagizwa. Wanalaza Amina kitandani nakuanza kumshugulikia. Baada ya msaa manili anaanza kujitingisha)

**Muuguzi** — Wacha niwaite wazazi wake. (wanaingia ndani)

**Daktari** — Ni mewaita kuwaambia kwamba msiwe na hofu tunapiganisha kadiri tuwezavyo. Na sasa hivi mtoto anaaza kujitingiza. Sasa ningetaka mzee arudi kuwachunga wengine watoto nyumbani, halafu mama abaki na mtoto hapa tunapozidi kumshugulikia. Atapona nawahakikishia, msiwe na hofu, muwe na tumaini.

## ONYESHO LA PILI

(Nijioni, Mwalimu anatembea barabarani na kukutana na mzazi na wanaendelea pamoja huku wakizungumza)

**Mzazi** — Habari za mchana Mwalimu, nafurahi kukuona.

**Mwalimu** — Sina habari mwenzangu. Zote za huzuni.

**Mzazi** — Kuna nini tena?

| | |
|---|---|
| Mwalimu | Ah, kwani wewe mgeni hapa Masisi. Hujui yanayoendelea mjini? |
| Mzazi | Najua lakini vituko vimekua vingi kwamba nashindwa kutofautisha. Nipashe. |
| Mwalimu | Majeuri yamezidi nchini. Wahutu wameitesa Congo kweli. Jana kabisa nilihuzunishwa na kushituka kusikia mwanafunzi wangu wa Chekechea, Amina, kabakwa na watano... |
| Mzazi | Eti nini? Eeeh! hiyo ni mikoshe. Mungu wangu! Je huyo mtoto hakufariki. Watu gani hao ambao wameanza kuwatendea watoto namna hiyo? |
| Daktari | Ni janga na shida ya kila mwana Masisi. Tumeshindwa la kufanya. mtoto hakufariki alipelekwa hospitalini na, nimesikia leo alianza kuongea... |
| Mzazi | Afadhali, Mungu nimkuu kuona bado anapumua. Maulana anabariki hao Madaktari wenye wanajitolea kuokoa maisha ya watu wetu waliojeuri. |
| Mwalimu | Madaktari kweli wanajitolea wawezavyo lakini nimesikia hospitalini hawana hata dawa. Zote walizokuwa nazo zimeisha na pesa hawana kununua vifaa vya matibabu Nchi yetu kweli sijui tunaelekea wapi, ufisadi |

na majeuri umezidi. Wafanya kazi wote hatulipwi vizuri. Kwanza mishahara yenyewe kidogo na hulipwa nusu nusu.

Mzazi: Ala serekali yetu nayo, wanaotuongoza hawagundu-wi kuwa nchi yetu inakumbana na shida nyingi kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Na mbona si muda mrefu uliopita serekali ilisemeka kukopa dola millioni tano kutoka Ulaya. Nashanga hizo pesa zote zilifanya kazi ipi kama bado wafanya kazi hawapokeyi.

Mwalimu: Hmm, hao viongozi siniwezi na wanyanganyi hao. Kwanza shida nyingi tunazo leo hapa ni kwa sababu ya uongozi wao mbaya. Hizo pesa walizila nakudai zilifanya kazi. Kama zilitumika mbona barabara ziko tabani wala shule kutokua na vitabu. Ufisadi unatutawala. Ndugu unajua shida iliyopo ni kwamba wanatwika kizazi kijacho na madeni. Hapo nchi itaendeleaka lini kama itakuwa natumikia kulipa madeni?

Mzazi: Gundua kuwa viongozi wetu wengi mamlaka walipata siokwamba walipita uchaguzi. sinakumbuka wizi wa kura uliripoti wakati wa uchaguzi. Wanapesa zao, nahapa pesa ni mamlaka. Kwanza najua hiyo

dala millioni tano wameikopa sababu uchaguzi umekaribia. Kumaanisha walizimweka mfukoni mwao kwaajili ya kuiba na kununua kura ndio waendelee kujidumisha mamlakani. Mara hiyi wananchi tuwe macho mpango yao usifaulu. Mwalimu nyinyi ndio wasomi, tunawatazamia kusimama na kutetea haki za wanyonge na kuokoa nchi yetu.

Mwalimu: Mara hiyi hawatafanyikiwa. Tangu nchi tupate uhuru kutoka mkoloni, tumekua tukipitia matatizo mengi. Sasa ni wakati wakati wakuinuka. Hilo ndilo wazo ninalo pia ninajaribu kupata mtu mashuuri ambaye tutaungana mkono ili tuanze kampeni ya utetezi haki zetu. Nimesikia kuhusu uwajibikaji wa Daktari. Nafikiri itabidi nimwone ilituzungumze kiupana kuhusu mpango huo. Najua atafurahia hilo, kwanza nimesikia madaktari pia wamekatwa mshahara sana na unacheleweshwa sana.

Mzazi: Mjitahidi kabisa, tuko nyuma yenu na tutawasaidia kwa kila jambo mpaka haki ifanyike. (wanaagana na kila

mmoja kuenda njia yake.

## ONYESHO LA TATU

(Ni jioni, Daktari anaketi sebuleni mwake na kutaza muktasari wa habari kutoka BBC)

BBC " Naam, mpendwa msikilizaji mahali popote ulipo karibuni kwenye muktasari wa habari wa jioni ya leo. Tukiwa na saa kumi unusu kulingana na saa za kimashariki. Umeletewa na wako mtangazaji Ben Bella.

Habari kamili; mkuu wa jeshi la jamhuri ya kidemokrasia ya Congo; jenerali Didie Etumba ametangaza kuanzisha rasmi kwa opereshen, zidi ya kundi la waasi wa kihutu kutoka Rwanda, FDLR mashariki mwa Congo. Lakini jeshi la umoja wa mataifa, MONUSCO ambalo ndilo mshirika wake mkuu katika vita zidi ya makundi wenye silaha eneo hilo. linasema halijaanza mashambulizi bali liko katika matayarisho muhimu kabla ya kutekeleza uamuzi huo.

Uamuzi huo wa Didie Etumba unatokana na maongezi yaliyoendelea baina ya viongozi wa kundi la waasi; serekali ya Congo.

na wawakilishi wa umoja wa mataifa. Wahutu walihitajika kusalimisha bunduki, kuacha ujeuri na kurejeshwa kwao Rwanda kwa njia ya amani. Kutoka maelfu waliokatika misitu ya nchi ya Congo, 280 pekee ndio waliojisalimisha huku wengi wakidai hawawezi kurudi Rwanda sababu walihitaji wahakikishiwe usalama wao kupitia maongezi na serekali ya Rwanda, jambo ambalo Rwanda imekataa. Kumbaka mpendwa msikilizaji kwamba waasi hao walikimbia kutoka Rwanda mwaka wa 1994 kufuatana na machinjo zidi ya watusi ambapo watu takribani laki nane walipoteza maisha yao, huku wengi wakibaki wajane na mayatima.

Sasa mpendwa msikilizaji, inaoneka kuna utofauti kufuatana na kauli ya kukabiliana na waasi hao. Kwanza baina ya wakongomani na viongozi wao na baina baina ya jeshi la Congo na umoja wa mataifa.

Wakongomani wamesema hawawezi kungoja ila kuwashambulia waasi hao mara moja kutokana ubakaji na uhalifu wamekua

wakitendea Wakongomani karibuni miaka ishrini sasa. Generali Didie Etumba anafuata maoni ya wana nchi huku viongozi na umoja wa mataifa wanaendelea kubembeleza wahutu watoke kiamani. Jambo sasa wakongomani wanasema limekuwa likifanyika miaka nenda miaka rudi bila mafanikio. Vile vile wana Congo, wengi wanamshutumu raisi wao nakusema kuwa yeye ni Munyarwanda na amekua akitumia ufisadi kujidumisha mamlakani. Endapo kunautofauti katika kauli za kukabiliana na waasi hao wana nchi wameamua haswa wale wa mashariki ambao wanateseka sana; kukiwemo miji miwili Goma na Masisi ambapo wanawake ishrini hubakwa kwa siku na hao waasi. Naam sasa, mpendwa msikilizaji hapo tumefikia mwisho wa kipindi cha taarifa ya jioni ya leo. Kumbuka umeletea na wako mtangazaji Bene Bella. Asante na jioni njema."

(mlango unabishwa, Daktari anajizindua kutoka kitini na kuenda kufungua. Anakuta ni rafiki yake wazamani Mwalimu)

Daktari (akitabasamu kwa furaha) oohooh! rafiki karibu sana tena sana nyumbani kwangu.

| | |
|---|---|
| Mwalimu | Asante rafiki, siku nyingi. Tangu tulipomaliza shule hatujaonana. Muda mrefu sana. |
| Daktari | Ukweli na ndio sababu ninafuraha ghaya kukuona leo. Wewe na jamii lako hamjambo |
| Mwalimu | Hatujambo kaka sababu bado tunatembea na kupumua. Siunajua mwenyewe vile hali ilivyo hapa Masisi. Vipi wewe? |
| Daktari | Nafurahi kusikia hivyo. Mimi vile vile mzima kama unavyosema sababu ya kupumua tu. Uhalifu sasa umevuka mipaka. Sasa hivi nimekua ni kitazama taarifa ya habari, 'BBC kulingana na vile mambo yanavyozidi kimeenda mrama ... |
| Mwalimu | (akimkatiza) oh nafurahi kama nawe umetazama hiyo taarifa. Hata nami mbele nije nimekuwa pale mkahawani nikitazama. Nisikitiko kubwa rafiki. Hata hivyo nimekuja leo ili tupate kuongea vile tutashimama na kutetea haki za watu wetu. Hatutangoja sasa, tumeteseka sana. Wake, watoto na mali zetu zimeharibiwa. Lazima, lazima.... |
| Daktari | Asante rafiki, yaani umeningia kwenye mawazo; huo ndio mpango niliokuwa nao. Wajua tumeona mengi lakini yale yaliyofanyika majuzi kwa mtoto Amina, hilo limenisisimua. Isitoshe, dawa za matibabu hatuna katika |

hospitali. Inamaana kwamba watu wetu watazidi kufa kwa ubakaji, njaa na magonjwa. Kama vile Daktari naweza kukuhakikishia kwamba 80% ya wale ambao wamebakwa huwa na virusi vya ukimwi. Huo ni utafiti mwenyewe nimefanya. Ikimaanisha kwamba katika miaka michache ijayo tutapoteza watu wengi kulingana na hali mbaya ya matibabu.

Mwalimu: Nashukuru sana mpendwa, tutajitahidi kufanya tuwezayo na kulilia viongozi wetu watusaidiye. Labda katika wiki ijayo tutawaitisha watusikize.

Daktari: Wazo nzuri, lakini hawawezi kutujia lazima sisi tuwaendee. Endapo ninashughuli nyingi hospitalini, nitapata muda sababu tunachokiendea ni muhimu sana.

Mwalimu: Asante sana kaka, tutazidi. Kwa heri.

Daktari: Ya kuonana!

ONYESHO LA NNE

(Hospitalini Masisi, Daktari anaonekana mwenye kuchanganyikiwa. Anajizungumzia huku akizunguka zunguka ofisini. Anakuta barua mezani na kuanza kuisoma)

Daktari: (Kwa mshituko) la! oh, haiwezekani. Nifanyeje? (anachukua simu na kumpigia

| | |
|---|---|
| | Mwali ) Halo! |
| Mwalimu | Ndiyo halo! mambo vipi? |
| Daktari | Hamna ndugu yangu, mambo hayaendeki hata kidogo. Yaani - - - |
| Mwalimu | Tafadhali niambiye, tusaidiane - - - |
| Daktari | Ni kwamba nimechanganyikiwa na ninacho-kipata asubuhi hiyi barua ambayo imenitarifu kwamba wafanya kazi wote Hospitalini wamekimbia kazi. Kwa hivyo, nimebaki peke yangu na haya mamia ya wagonjwa tabani. Nimeshindwa la kufanya kabisa... |
| Mwalimu | Mungu wangu! mbona mbona wakachukua uamuzi kama huo? |
| Daktari | Sababu kamili ni kwamba wiki chache zilizopita wafanya usafi walijifuta kazi, hawakukua wamelipwa miezi mitatu yote huku wakindanganywa. Pia kilicho fanya wengine wakimbie, maji yalikatwa, eti hatujayalipia. Je unanifuata? |
| Mwalimu | Nakufuata, endelea. |
| Daktari | Hospitali imekua vibaya sana kwa ngambo ya usafi tangu hapo. Hua umekua mzigo mkuu sana, kushughulikia wagonjwa pamoja na kutafuta maji. Kama nilivyokuambia Hospitali imeishiwa dawa na kila siku |

tunapoteza watu sababu ya hilo. heo hata sijui wangapi wameaga.

**Mwalimu:** (Anaitikia na kusikiliza kwa uchungu sana)

**Daktari:** Wauguzi na wasaidizi wote waliacha kazi sababu ya vifo vingi walivyoshuhudia. Sio eti tunakosa ujuzi wakuwatibu bali vifaa hakuna kabisa jambo lililofanya hata wale wachache waliokuwa wamejitolea, kuacha ni kwamba tulishindwa na chakula, pamoja na kukatiwa stima. Hospitali sasa inanuka vibaya sana, hata hapo ofisini mwangu harufu imezidi. Nimeshindwa kuamua nitafanya je kuhusu hawa wagonjwa.

**Mwalimu:** Siwezi kustahimili haya ndugu, wacha nije mara moja huko. Siwezikuachilia, niko tayari kuacha kazi yangu ya walimu tusaidie watu wetu sababu hata shule kwenyewe hakuna tunachokifanya, hatuna vifaa. Watoto nao hawaji tokana na njaa na shida katika jamii zao.

**Daktari:** Asante mpendwa, bwana akubariki sana. Umefanya vema sana. Umenitia moyo sana. Basi, uje halafu tuone tutayapeleka je.

**Mwalimu:** Nimejawa na wazo. Hebu niwaite vijana wangu watatu, niwape vipaza sauti na kutangaza mijini mwote vijana na watu wajitolee tusaidiane sote.

**Daktari:** Hongera! Mwalimu hiyo ndiyo sababu umoja ni nguvu. Hayo ndio nakupendeaka, mawazo

ambayo yamekomaa. Hata we pia usije sasa hivi. Wafuate hao sababu nakuamini unamaneno matamu ya kusadikisha watu wasaidiye. Sio lazima watu wote waje hapa. Wale ambao hawana nafasi ya kuja; wacha watoe maji, chakula, kuni ama hela endapo najua hivo ni, haba hapa kwa hali tulionayo. Hata mimi ningependelea tuwe sote lakini hakuna jinsi naweza kuacha hospitali pekee.

Mwalimu: Asante kwa hayo mawaidha, Nitashughulikia hayo sasa kabisa, siunanijua tu. Usiwe na wasiwasi watu watatokelezea hapo mnamo dakika chache.

Daktari: Nilikuwa nimewajuza baadhi ya marafiki wangu ngambo kuhusu mateso tunayopitia, na sasa naona ujumbe wa pepesi, ukiniarifu kuna watu kadhaa wenye huruma ambao wametutolea pesa za kununua dawa ambazo zitatusaidia kwa miezi kadhaa. Watu wakarimu sana bwana awabariki!

Mwalimu: Alhamdulilahi! wabarikiwe zaidi. Hilo lina nitia moyo. Ndugu tukazane hatuko peke yetu endapo giza limejaa kila mahali. Watu hao wamejitolea sababu wanatuchukua kuwa ndugu binadamu ambao sote tuna mwelekeo mmoja. Basi tuzidi kuwa na matumaini, na

| | |
|---|---|
| | mengi bado yako njiani. |
| Daktari | Isitoshe nimepata ujumbe mwingine wanaletutolea Lori la wahindi na maharagwe. Kumaanisha tutakuwa na chakula, kuanzia kesho. Nafurahi sana hata kama huu msaada hauja kuwa ndio suluhisho kamili la matatizo yetu, ila utatusaidia tunapoendelea kupiganisha. Utanipigia basi baadaye na kunijulisha kunaendaje. |
| Mwalimu | sawa, baadaye. |
| | (Anakata simu nakuwaita vijana wake. Wanaongea kwa dakika chache halafu wanatoka kutangaza) |
| Matangazo | " Halo! Halo! kwa wazalendo wote na wana Masisi wote. Kwa baba, mama, ndugu na dada unayenisikia. Ndimi wenu Mwalimu nikishirikiana na Daktari pamoja na washirika wengine. Kama mnavyojua tumeyapitia mengi, shida na matatizo zimetukumba hatujui tukimbilie wapi. Bali tulipo sasa ni kwamba tumetoka kwenye kikaango na kuingia kwenye moto wenyewe. Wafanya kazi wa hospitali yetu wote wameacha kazi kufuatana na dhuluma ya mishahara yao. Hebu fikirieni kulihusu ni jambo ngumu sana. Ni tatizo tokana na ujeuri na magonjwa yanayotukumba. Kama hospitali haifanyi kazi inamaana sote tunaisha. Hao ndugu zetu ambao wanalazwa watakuwaje? |

Ni kwamba tunataka watu wajitolee. tusaidiane bila kutarajia mshahara sababu serekali yetu imejawa na ufisadi, tukisema tutaupwa ni sawa sawa na kujidanganya wenyewe. Hatutaki kudanganyana. Ni wakati wa kusema kweli. Wakati ambapo kila Mwananchi anapashwa kusimama na kuwasha nuru. Natunawashaje nuru? Ni kujitolea kwako baba, mama, ndugu na dada sasa hivi. Kwenda hospitalini na kusaidia wananchi wengine ambao wako katika hatari ya kufa. Ni kupitia mchango wako wewe ambaye hauwezi kufika hospitalini sasa. Haijalishi kama ni chakula, pesa, maji au chochote ulichonacho. Kuna vijana ambao tayari wako huko nje kusanya matoleo yenu. Fimbo ya mbali haiuwi nyoka, wacha tutumie tuliyonayo leo hata kama ni haba. Haba na haba hujaza kibaba, usisumbukie kesho, itajisumbukia yenyewe. Nakuhakikishia kwamba tutaleta mabadiliko endapo tutaungana mkono. Pamoja tutawasha nuru na kupinga hata uongozi mbaya tulionao sasa. Jamani, tutaka chini hadi lini? Situote mbawa na tuanze kuruka. Ishara za onyesha

mnasikia. Asanteni sana sote tupamoja na umoja ni nguvu."

Daktari (anapigia Mwalimu simu) Halo! Ubarikiwe sana hongera kabisa. Kazi njema, yaani hapa sasa nina karibu watu hamsini ambao wako tayari kuchapa kazi. Hakika nashukuru kwa kazi uliyoifanya, vyakula, maji na mengine ya metiririka kabisa.

Mwalimu Huhitaji kunishukuru ndugu, nilitekeleza wajibu wangu kama mzalendo. Nashukuru kama hao waliojitolea. Vijana bado wanaendelea kupacha habari na kusanya yanayotolewa. Mwenyewe naja tusaidiane.

Daktari Haya safi kabisa.

ONYESHO LA TANO

(Ni juma tatu asubuhi, Daktari na Mwalimu wako tayari kwa mkuu wa mji wa Masisi wakingojea wawakilishi wa viongozi ili kusumulia shida na matatizo ya nchi)

Daktari Leo hakika tutafanya juu na chini viongozi wasikiye vilio vyetu ndio serekali itusaidie.

Mwalimu Mengi yamefanyika na tuwaelezea wazi wazi huenda wakatega sikio.

Daktari Tungojee tuone vile yataendeka, lakini sikio la kufa halisikiyi mvua. Karibu waje

muda umekaribia.

(wawakilishi wa viongozi wanafika na kuketi upande waliotayarishiwa. Wanafuatiwa na askari wanne, wawili mlangoni wengine wawili upande wakulia na kushoto wao)

**Mnenaji** Haya tayari naona washika dau na wahusika wote tupohapa. Kwa hivyo ningependelea, Askari atuongoze tuimbe wimbo wataifa kwa kuoko muda ndiposa tuanza mazungumzo.

(wote wanasimama na kuketi pindi wanamaliza kuimba) Haya basi nyote mnakaribishwa kwenye hichi kikao cha leo na ningependelea kila mmoja awe huru na mjasiri kujieleza Mimi ndiye Mnenaji wenu leo pia hapa ninakamati ya wawakilishi wengine wa viongozi Kwa hivyo ningependelea ni wapeye pia nafasi kujitambulisha.

**Daktari** Asanteni sana. Mimi ni Daktari na hapa nina mwenzangu Mwalimu. Sote tunashiriki na pamoja katika kusaidia wananchi wenzetu Tunashukuru kukubali mwaliko wetu, natumai kwamba tutasikizana na kufikia suluhisho la shida tulizo nazo.

**Mnenaji** Nafikiri kila mmoja amejitambulisha. Tupo hapa kufuatana na ombi lenu la kuzungumza nasi. Mtaenda kutoa malalamishi yenu, nasi

tunatoa maoni yetu. Karibuni.

Daktari: Asante. Sisi tuko hapa kuwaletea matatizo yetu na vilio vyetu. Kitu ambacho nafikiri mnafahamu sababu nyinyi ndio viongozi na mnapachwa kujua yale watu wenu wanapitia. Nyinyi ndio baba zetu nyinyi ndio mnapashwa kutusaidia. Lakini imeonekana kwamba nyinyi mlikosa kutekeleza wajibu wenu ndio sisi tukaja hapa. Mimi ni Daktari na mwenzetu hapa ni Mwalimu, hatuhusiani na uongozi ila baada ya kuona kile ndugu zetu wanateseka tukaamua kuwasimamia. Mbele niingilie mengi na washutumu kwa kutowajibika kama viongozi. Huu ni wakati nchi inahitaji mtu anayetazamiwa kusimama na kuwahimisa bali hata mmoja wenu hajafanya hivyo.

Mnenaji: Subiri kidogo bwana, unataka tufanyeje? Tuje tukeshe manyumbani mwenu ndio muone kuwa tunawajibika. Lazima muwe nashukrani, hiyo ndio shida ya watu, kulalamika lalamika tu bila kuona mema wanaofanyiwa. Kama hatungewajibika hamngetuona leo. Kwa hivyo utaachana na hizo stori na mtuambie shida zenu nizipi.

Daktari: Hilo ambalo ninaligusia mheshimiwa, ni moja ya shida zetu. Nakumbuka kwamba mimi nawakilisha wenzetu, kwa hivyo tutakubaliana

Kwamba nitasema maoni ya wananchi haijalishi, kama yanawachukiza. Katika maswala tuliyonayo ni ubakaji ambao umekuwa ukienezwa na waasi wa Kihutu (FDLR). Hili ni jambo sote tunafahamu na tunachohitaji kufanya ni kufikia suluhisho. Watu wanateseka sana, karibuni kila siku hatukosi visa vya ubakaji; vitendo hivi vya kinyama vimetuchosha. Hawa hawa ndio wanao tuua, na kupora mali zetu. Watu wengi hivi leo wana njaa sio eti hawakukuwa na chochote bali kaporwa.

Mnenaji: Poleni kwa wale ambao wameathirika, tunafahamu hayo natunajaribu kuyashughulikia.

Mwalimu: Vema kama mnafahamu haya, lakini mheshimiwa mpaka lini mtashughulikia hayo na kuleta suluhisho. Sababu hali imekuwa hivi kwa miaka na watu wanaishi

Mnenaji: Mnapashwa kuelewa kwamba hatuketi chini tunafanya tuwezalo bali kutatua shida hiyi sio rahisi vile tunaweza fikiria, ama maoni yenu ni yapi kufuata kutatua haya?

Mwalimu: Suluhisho hapa ni moja bwana, mtulinde tokana na waasi wa Kihutu (FDLR).

Shabaha ya kwanza ya serekali ni kuhakikishi a raia wake usalama. Endapo sio rahisi vile lakini kiongozi wa ukweli ni yule ambaye hua tayari kutoa maisha yake kwaajili ya anaowaongoza. Kama mmeshindwa kupiga na kurejesha FDLR kwao si wakabizi silaha zao halafu waishi kwa amani pamoja sote. Tunajua kwamba wao hudai kwamba hawawezi rudi Rwanda tokana na kuhofia usalama wao. La kushangaza ni kwamba wao wanajua umuhimu wa usalama wao lakini sio wa watu wengine. Sasa viongozi mjifikirie sababu tunalotaka ni usalama wetu, mali zetu na vizazi vyetu vijavyo. Maoni ya 80% ya wananchi ni kwamba hatuwezi pata usalama pindi FDLR bado ako katika misitu ya Congo na silaha zao. Yale walioyafanya kwao Rwanda miaka 20 iliopita ndio waliendeza hapa kwetu. Ujeuri uko katika damu yao.

Mnenaji: Tumesikia hayo. Tutajaribu kuyatilia maanani. Kila moja anashida zake hata sisi wenyewe. Mnamalalamishi mengine zaidi ya hayo?

Daktari: Bado mengi. Tuna uchungu mwingi kuhusu ubakaji, karibuni 85% ya wale wenye wanabakwa huambukizwa virusi vya ukimwi. Magonjwa na janga la njaa la kumba wengi nchini.

Hivi tunavyoongea tuna mamia ya wagonjwa katika hospitali yetu licha ya kwamba tumeishiwa na dawa watu wengi wanakufa sio eti yakukosa huduma ya madaktari bali dawa na vifaa havipo. Miezi michache iliyopita mliahidi kutotoa pesa kushughulikia hayo, na hamkulifanya. Wiki iliyopita karibu tufunge hospitali sababu tulikatiwa maji, umeme na ukosefu wa chakula. Endapo kuna msaada kidogo tumepata kutoka marafiki. Tunawaomba mtulipie matibabu na mlipe pia wafanya kazi wote walioacha kazi sababu ya kudhulumiwa mishahara yao.
Ni jambo la kusikitisha sana vijana wengi hawaendi shule. Tuna shule za kutosha hapa lakini nyingi zimefungwa sababu wazazi hawana pesa za kulipa karo. Hivyo ni hitaji letu kwamba serekali ieze kulipia watoto masomo. Hao ndio nguzo za nchi yetu, ndio kesho ya Congo. Uchumi wa nchi nao umeshuka chini kabisa ila bado kila mwezi munatupunguza mshahara. Garama ya maisha imepanda sana, itakuwa vema kama hata mnatafuta kazi kwa ajili ya wale ambao hawana.
Nchi yetu tajiri sana kirasili mali lakini nyinyi viongozi pekee ndio mnao faidika. Tuambiane kweli, nina watoto tano nawote wameacha shule sababu ya kukosa karo, ila nina uhakika kuwa watoto wenu wako shule na wana chakula. Kitambo wengi tulifaidika kutokana na uhuru wa kuchimba madini, lakini sasa

mnawakataza watu na kuleta kampuni za ugenini ambazo zibeba mali yetu yote kujenga nchi zao bila kurudishia jamii vya kutosha. Tunawaomba tuendelee kuchimba almasi, fedha, dhahabu na madini mengine kusaidia jamii zetu. Jamuhuri ya kidemokrasia ya Congo ni nchi ambayo ina vitu vingi viaajabu. Kimaumbile ambavyo vya weza kutufaidi sote kama uongozi unajipanga vema na kupunguza ufisadi. Ningependa kumalizia kusema kwamba serekali pia iache kutumia vitisho kunyamanzisha malalamishi ya watu. Mwaka huu visa vingi vimeripotiwa rahisi akituma askari na kuua waadamaji. Nkumbuke kuwa nchi yetu huitwa Demokrasia ya Congo. Demokrasia ambao ni uongozi wa watu, na watu kwa watu.

Mnenaji (anataza karatasi aliyoandika) Tumesikia malalamishi yenu ila mfahamu kwa hatunyamanzi. Tunasaidia endapo hamuoni hivyo, kama hatungekuwa tunafanya chochote wote mngekuwa mmeisha. Tunamipango kabambe wa kazi kwa wote na malipo bora. Tutasomesha watoto wote, muetu na subira. Matibabu yatalipwa pia, pesa ambazo zingelipia matibabu rahisi alizikopa kumupeleka mamaye kupata matibabu ulaya na akamnunulia nyumba akae huko sababu angerudi hapa angezidi kuzohofika. Hiyo ndio dharura ilifanya tusitowe hizo pesa. Bali nafikiri zilifanya bado kazi ya matibabu katika kusaidia mama raisi.

swala la usalama bado changa moto lakini tushirikiane tu. swala la madini sisisi wenyewe ndio tuliamua yachimbwe na kampuni za kigeni. Hamuwezi kupinga hayo yaliyoamuliwa na wakuu wenu, ni lazima mtuheshimu nasi tuwaheshimu. Hivi karibuni kila mtu atakuwa sawa, lakini lazima mtushukuru sababu tunayofanya hapa Congo haifanyiki kila mahali. Mipango tuliyonayo haiko katika kila nchi labda zile chache zilizoendelea. Sasa mnaporudi kwa watu mwajulishe kuhusu juhudi zetu. Mtuwakilishe kwa viongozi wa kupigiwa mfano.

Daktari: Mheshimiwa kwa maneno mingi huwa hamna shida. Kutuahidi nyingi huwa haraka sana lakini shida yenu ni kutekeleza. Sasa hivi hamuwezi kudanganya wananchi wala wao kuwasadiki. Mmewadanganya vyakutosha. Huu ni wakati wa vitendo sio maneno tu. Hivi mnavyotuambia leo sio ajabu hata mjukuu wangu kuzaliwa na hayajatekelezwa. Vitendo huwena zaidi kuliko maneno.....

(mkutano unaisha; Daktari na Mwalimu hawana furaha lakini wawakilishi wa viongozi wanaenda wakicheka na kuongea)

ONYESHO LA SITA

(Daktari ombeni, Mwalimu, mama mashauri na sauti

ya wanawake, wanakutana. kuzunguza na kutiana moyo)

Daktari: Hamjambo mama na dada zetu!

Sauti mama: Hatujambo ndugu yetu wa samani!

Daktari: Kwangu ni jambo la kufurahisha kuwaona wamama wengi hapa Masisi wamekusanyika kushirikiana na timu yetu tunaopiganisha haki ifanyike. (wanapiga makofi, nderemo na vigelegele)

Daktari: Sote tunajua vile hali ilivyo nchini; ubakaji, ukora, ufisadi, magonjwa na njaa. Tumejaribu tuwezavyo kurekebisha hali bali bado hatujafikilia lengo letu. Tumeongelesha viongozi wetu ambao ilikuwa vigumu wao kutusikia tokana na ufisadi na ubinafsi wao. Tujue hata hivyo kuwa mambo yote iko mikononi mwetu. Sisi ndio tunaweza leta mabadiliko, ndiposa leo tutajadili kuhusu mipango tunayo inayosaidia kuyaleta. Napenda kusikia wamama wanafanya nini vile vile kujisaidia. Mama wa shauri atuongoze katika huu mjadala tafadhali!

Mama shauri: (wanamshangilia na kupiga mikono anaposimama) Nafurahi sana kuwa mbele zenu ndugu na dada wapendwa. Kulingana vile tunavyoishi leo kama vita na ubakaji vinaisha, sisi wanawake wa Congo tungali tutainuka na kungaa. Kufanya kazi zozote zile kama wanawake wengine mahali popote ulimwenguni ili kusaidia jamii zetu na kujenga nchi yetu.

Daktari: Maoni mzuri, tunapenda tusikie mpango wenu kuhusu kujiokoa na hali tulionayo.

Mamashauri | Tumeanza na kufanya muungano wa wamama ambao nausimamia. Tunajitolea kutumika pamoja sababu umoja ni nguvu. Tunafanya kazi za nguvu na za kujitolea ili tusaidiane. Huenda shambani katika makundi na hilo hupunguza uoga na visa vya ubakaji wakati mwingine. yaani, tunashirikiana kwa hali na mali.

Mwalimu | Kama wanawake ningependa nijue huwamnahisi vipi kulingana na vitendo hivi vibaya.

Mamashauri | Hujihisi vibaya; kwa tumeonewa, kuzarauliwa na kutukanwa. Hiwa ni aibu kubwa na kama ungejua wengi hubakwa na kushindwa kusema, hasa wale walio na waume huhofia kukataliwa. Sasa tunachofanya kama kikundi ni kuwekana moyo na kuhimizana kusonga mbele bila kuangalia tuliopitia. Leo hiyi, hapa kwetu Congo ndipo mahali hatari sana kwa mwanamke.

Daktari | Masisi ni kubwa, mnafanyaka namna gani kufikia wanawake wote hapa?

Mamashauri | Kikundi chetu kimekua kizito na hivi sasa hakisimamii hapa tu, kimesambaa sehemu mbalimbali hapa Congo. Najua kwamba wakati wote nchini tutafikilia huo umoja tutaleta mabadiliko. Tuko na wawakilishi na washauri wa wamama hata katika mapori. Jambo kienda mrama wao hutupasha ili tusaidiane. Hapa majuzi dada yetu Masumbuko, alibakwa na askari wanne huku akiwa na mimba ya miezi sita. Hali ilikuwa nzito na haingekuwa msaada wa hao

wenzetu angekufia huko Porini. Hao washauri walimchukua na kumleta hospitalini ata kama alipoteza mimba na kuambikizwa ukimwi bado yu hai.

Mwalimu Nashangaa mnafanya nini kuhusu watoto wenu wakati mnahayo majukumu yote. Ni swala sote tunapashwa kuangalia sababu watoto ndio kesho.

Mamashauri Hilo ni jambo la kimsingi katika malengo yetu. Tunajaribu. Nchini sasa yatima ndio wengi sababu wazazi wameuliwa au kulemezwa. Kutokana na hayo kikundi chetu kilijenga kituo cha mayatima na wale wamama ambao wamejeuriwa na wanahofu kuishi pekee. Kazi zetu shambani hunalisha hao wote. Endapo tunajaribu changa moto ni elimu, tunatazamia serekali kwa hilo, letu ni kuhifadhi maisha kwanza.

Daktari Bila elimu kwa hao watoto bado itakuwa vigumu sana kufikia malengo yetu na kuimarisha jamii yetu. Tuna moyo wa kuzidi kupiganisha ila bado mengi bado ya kuimarisha katika nchi ya Congo...